# HALMASHAURI YA WILAYA YA SIMANJIRO

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 27.10.2021 KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIMANJIRO

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

1. Mh. Baraka Kanunga Laizer - Mwenyekiti wa Halmashauri
2. Mh. Sendeu Korduni Laizer - Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri
3. Mh. Loishiye Lesakwi Laizer - Mjumbe
4. Mh.Jackson L. Sipitieck - Mjumbe
5. Mh. Jacob Kimeso Lukendo - Mjumbe
6. Mh. Rehema Zanaki Laizer - Mjumbe
7. Mh. Christopher Ole Sendeka (MB) - Mjumbe

**WAJUMBE AMBAO HAWAKUHUDHURIA**

- Hakuna

**MWALIKWA**

1. Mh. Jackson Materi - Mjumbe wa Kamati za Huduma za jamii

**WATENDAJI WALIOHUDHURIA**

1. Samwel W. Gunzar - Mkurugenzi Mtendaji (W)
2. Boniphace J. Mhabe - Kaimu Afisa Usafi na Mazingira
3. Dkt Aristides Raphael - Mganga Mkuu (W)
4. Paulo Daati - Kaimu Afisa Uchaguzi
5. Linus Mboya - Mtakwimu
6. Anold Munisi - Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
7. Marwa Christina - Afisa Utumishi
8. Gasto S. Silayo - Afisa Utumishi na Utawala (W)
9. Dkt Edward Ole Motika - Daktari wa macho
10. Daudi Lukumay - Kaimu Afisa Usafirishaji (W)
11. Iddi A. Ibwende - Kaimu Katibu TSC (W)
12. Heri Kuria - Afisa Mipango (W)
13. Silvanus M. Tairo - Afisa Elimu Msingi (W)
14. Asia Ngalisoni - Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii (W)
15. Louis M. Mwenempazi - Mwanasheria
16. Edosi E. Ndikwiki - Afisa Tarafa Ruvu Remit
17. Evence M. Mbogo - Afisa Mtendaji Mji mdogo Mirerani
18. Oscar A. Pessa - Mkaguzi wa Ndani



CamScanner

19. Lonyamal N. Kivuyo - Kaimu Mkaguzi wa Ndani (W)
20. Eng.Fabian Malagila - Kaimu Afisa Kilimo na Umwagiliaji (W)
21. Cedrick S. utou - Kaimu Afisa Ugavi (W)
22. Baltazari J. Sulle - Afisa Ardhi na Maliasili (W)
23. Tumaini Sebastian - Afisa Tarafa Naberera
24. John M Wambura - Afisa Tarafa Msitu wa Tembo
25. Gosbert Magelanga - Mhasibu
26. Mkama Musese - Kaimu Mweka Hazina (W)
27. Peter P. Sanga - Afisa Biashara (W)
28. Joseph K. Mtataiko - Afisa Tarafa Moipo
29. Peter C. Ibede - Mhasibu
30. Emanuel Mark - Afisa Utumishi
31. Yeniel Kagonji - Afisa Utumishi
32. Daniel Mahona - Mhandisi wa Ujenzi (W)
33. Amosi Mandago - TEHAMA
34. Joachim S. Soka - Afisa Mtendaji Mji mdogo Orkesumet
35. Salima A. William - Afisa TEHAMA
36. Crispin M.Kaijage - Kaimu Mwanasheria (W)
37. Lekishon Lengoye - Afisa Tarafa Terrat
38. Chausiku Qaymo - Afisa Tarafa Emboreet

**WATENDAJI AMBAO HAWAKUHUDHURIA**

- Hakuna

**WAALIKWA**

1. Mhandisi Paul M. Mabaya - Meneja TARURA

**SEKRETARIETI**

1. Alais M. Kurumet - Mwandishi wa vikao
2. Joshua Saitabau - Mwandishi wa vikao

**MUHT. NA. 1/10/2021 KUFUNGUA KIKAO**

Kikao kilifunguliwa mnamo saa 7:50 mchana baada ya Mwenyekiti kuwakaribisha wajumbe kwenye kikao.

**MUHT NA. 2/10/2021: KURIDHIA AGENDA ZA KIKAO CHA TAREHE 27.10.2021**

1. Kufungua kikao
2. Kuridhia/ kuthibitisha agenda za kikao cha tarehe 27.10.2021
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao kilichopita cha tarehe 14.9.2021



CamScanner

**Mh. Baraka Kanunga Laizer – Mwenyekiti wa Halmashauri** alihitimisha hoja hiyo kwa kuelekeza kuwa Mkurugenzi Mtendaji ahakikishe anatoa kiasi cha TSh. 40,000,000.00 kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya kujenga nyumba ya mwalimu wa shule ya Sekondari Kitwai mwezi Oktoba 2021.

## MUHT NA. 9/10/2021: TAARIFA YA MANUNUZI ROBO YA KWANZA JULAI 2021 – SEPTEMBA 2021

**Afisa Ugavi (W)** aliwasilisha taarifa tajwa hapo juu iliyobainisha maeneo yafuatayo:-

A: Manunuzi yaliyofanywa na Halmashauri.

B: Manunuzi ambayo michakato yake haijakamilika.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kuipitisha kisha kuagiza yafuatayo:-

1. Mkurugenzi Mtendaji (W) afanye ukaguzi kwenye matumizi ya mafuta yaliyonunuliwa na Halmashauri kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2021 ili kuona kama yametumika kama ilivyopaswa.

## MUHT NA 10/10/2021: MAOMBI YA KUWEKEWA VIFUNGU VYA MATUMIZI NA MAOMBI MAALUM

**Afisa Mipango (W),** aliwasilisha taarifa tajwa hapo juu kwa kuelekeza kuwa Halmashuari ya Wilaya ya Simanjiro ilipokea kiasi cha TSh. 610,000,000.00 kutoka fedha za Kampeni ya maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya Uviko 19 kwa mchanganuo ufuatao:-

a) Ujenzi wa jengo la huduma ya wagonjwa mahutihuti (ICU) TSh. 100,000,000
b) Ujenzi wa nyumba ya watumishi wa Afya 3:1 TSh. 90,000,000.00
c) Ujenzi wa vyumba vya madarasa 12 katikashule za sekondari TSh. 240,000,000.00
d) Ujenzi wa vyumba vya madarasa 9 katikashule shirikizi TSh. 180,000,000.00

Aidha aliwasilisha mchanganuo wa fedha za miradi kama ifuatavyo:-

**A: Idara ya Elimu Sekondari**

| | |
|---|---|
| 1. Shule ya Sekondari Terrat darasa moja | TSh. 20,000,000.00 |
| 2. Shule ya Sekondari Shambarai darasa moja | TSh. 20,000,000.00 |
| 3. Shule ya Sekondari Simanjiro darasa moja | TSh. 20,000,000.00 |
| 4. Shuleya Sekondari Oljoro Na. 5 darasa moja | TSh. 20,000,000.00 |
| 5. Shuleya Sekondari Naisinyai darasa moja | TSh. 20,000,000.00 |
| 6. Shuleya Sekondari Naberera darasa moja | TSh. 20,000,000.00 |
| 7. Shuleya Sekondari Msitu wa Tembo darasa moja | TSh. 20,000,000.00 |
| 8. Shuleya Sekondari Tanzanite darasa moja | TSh. 20,000,000.00 |
| 9. Shuleya Sekondari Loiborsoit darasa moja | TSh. 20,000,000.00 |
| 10. Shuleya Sekondari Loiborsiret darasa moja | TSh. 20,000,000.00 |
| 11. Shuleya Sekondari Benjamin W. Mkapa darasa moja | TSh. 20,000,000.00 |
| 12. Shuleya Sekondari Emboreet darasa moja | TSh. 20,000,000.00 |
| | **Jumla TSh. 240,000,000.00** |



CamScanner

**Idara ya Elimu Msingi (Shule shikizi)**

| | |
|---|---|
| 1. Kandasikira – shambarai madarasa 2 | TSh. 40,000,000.00 |
| 2. Olmoti – Namalulu madarasa 2 | TSh. 40,000,000.00 |
| 3. Lengumumwa – Lemkuna madarasa 5 | TSh. 100,000,000.00 |
| | **Jumla TSh. 180,000,000.00** |

**Idara ya Afya**

**C: Jengo la huduma ya wagonjwa mahututi (ICU) TSh. 100,000,000.00**

1. Ujenzi wa jengo la nyumba ya watumishi wa Afya 3:1 katika Hospitali ya Wilaya TSh. 90,000,000.00

**D: MAOMBI MAALUM YA FEDHA**

Timu ya Menejimenti (CMT) imeomba kuidhinishiwa kiasi cha TSh. 16,100,000.00 kwa ajili ya shughuli mbalimbali kama ifuatavyo:-

1. Ujenzi wa uzio wa shule ya Sekondari Simanjiro TS. 15,000,000.00
2. Kuwezesha zoezi la uchaguzi wa chama cha watu wanaoishi na VVU Konga TSh. 1,100,000.00

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, wajumbe waliipokea na kuipitisha na kushauri kuwa uzio wa shule ya sekondari simanjiro ujengwe kwa kutumia matofali badala ya waya.

**MUHT NA. 11/10/2021: UJENZI WA KITUO CHA AFYA TERRAT**

**Mganga Mkuu (W),** aliwasilisha taarifa tajwa hapo juu, ambapo alieleza kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro ilipokea kiasi cha TSh. 250,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha afya Terrat. Pia alieleza kuwa Halmashauri ilipokea barua Kumb.Na. AC126/178/02/2/98 ya tarehe 24.09.2021 ya Mkoa inayotoa ushauri juu ya eneo la kujenga kituo cha afya Terrat kujengwa katika kitongoji cha shuleni ambapo kuna Zahanati ya Terrat badala ya eneo lililopendekezwa la Loondelemetie "A" kwa sababu zifuatazo:-

1. Ukaribu wa umbali kwa kilometa 2:9 kutoka Zahanati hadi eneo la Loondelemetie "A"
2. Uwepo wa udongo wa mfinyanzi katika eneo la Loondemetie "A" linaloweza kupelekea ongezeko la gharama za ujenzi.
3. Uwepo wa miundo mbinu katika Zahanati ya Terrat itakayopelekea kupunguza gharama za ujenzi.
4. Eneo la Loondemetie "A" lihifadhiwe kwa ajili ya matumizi mengine ya miundombinu ya jamii.



CamScanner

5. Mkoa kwa kushirikiana na Halmashauri upandishaji hadhi Zahanati ya Terrat kuwa Kituo cha afya baada ya miundombinu kukamilika.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kupitisha kisha kuchangia kama ifuatavyo:-

**Mh. Christopher Ole Sendeka Mbunge wa Jimbo la Simanjiro**, alishauri kupokea ushauri wa Mkoa lakini kuangalia mahali ambapo wananchi wametenga eneo la Loondelemetie "A" lijengwe kituo cha afya Terrat na gharama zitakazoongezeka wananchi watachangia.

**Mh. Jackson Materi Supeet – Diwani Terrat,** alitoa ufafanuzi kuwa wananchi wa Terrat wametenga eneo la Loondelemete "A" ijengwe Kituo cha Afya Terrat na wananchi wa Terrat wapo tayari kuchangia gharama yoyote itakayoongezeka.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kuipitisha kisha kuagiza kuwa;-

1. Mkurugenzi Mtendaji (W) ajenge Kituo cha Afya Terrat katika eneo la kitongoji cha Loondelemet "A" badala ya kujengwa kwenye Zahanati ya Terrat. Aidha wananchi wa Terrat wahamasishwe kuchangia gharama za ujenzi.

**MUHT. NA 12/10/2021: MAPENDEKEZO YA VIKUNDI VYA KUPEWA MKOPO**

**Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii (W)**, aliwasilisha taarifa tajwa hapo juu ambapo alieleza kuwa Kamati ya huduma ya mikopo Wilaya ilichambua na kujadili maombi ya mikopo kutoka kwenye vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu na kupendekeza kutoa mkopo wenye thamani ya TSh. 213,383,239:67 kwenye vikundi 36 kutoka kata mbalimbali Wilayani simanjiro kwa mchanganuo wa vikundi 8 vya vijana kupata TSh. 58,883,239:67 na vikundi 28 vya wanawake kupata TSh. 154,500,000.00fedha hizo zitolewe kwa mchanganuo ufuatao:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mapato ya ndani ya Halmashauri | TSh. | 70,013,396:72 |
| 2. Fedha za bakaa kwa mwaka 2020/2021 | TSh. | 9,252,946:07 |
| 3. Fedha za marejesho ya vikundi | TSh. | 134,117,053:95 |

Baada ya taarifa hiyo kuwasiliswa wajumbe waliipokea na kuipitisha kisha kushauri kuwa Mkurugenzi Mtendaji (W) aandae orodha ya vikundi vyote vilivyopewa mkopo na nakala ya taarifa hiyo wapewe Wah. madiwani wa kata zote ili wasaidie kuhamasisha vikundi hivyo kurejesha mikopo kwa wakati.



CamScanner

Ajira mpya (0), watumishi waliopo masomoni (19), watumishi waliostaafu (0), watumishi waliohama, watumishi waliofariki (3), watumishi wagonjwa(3), Watumishi waliohama / kuhamia (9) na taarifa za wakuu wa Idara/ Vitengo wanaokaimu (10).

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa wajumbe waliipokea na kuipitisha na kushauri kuwa wakuu wa Idara wanaokaimu ufanyike utaratibu wa kufuatilia ili wathibitishwe katika nafasi zao.

**MUHT. NA 18/10/2021 BANGO LA MKURUGENZI**

- Hakukuwa na Bango la Mkurugenzi Mtendaji (W).

**MUHT. NA 19/10/2021: MENGINEYO**

- Hakukuwa na mengineyo yaliyowasilishwa kwa mwenyekiti.

**MUHT NA 20/10/2021: KUFUNGA KIKAO**

Kikao kilifungwa mnamo saa 5:54 usiku , baada ya Mwenyekiti kuwashukuru wajumbe kwa michango yao, uvumilivu, na ushirikiano . Alisisitiza ushirikiano kwenye ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri.

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA**

| | |
|---|---|
| ........................................ | ........................................ |
| **KATIBU** | **MWENYEKTI** |
| 23/11/2021 | 23/11/2021 |
| **TAREHE** | **TAREHE** |



CamScanner